Basi tabia ya Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- ilikuwa ni Qur'ani

Amesema Sa'd bin Hisham bin Aamiri -alipoingia kwa Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake: Ewe mama wa waumini, nieleze kuhusu tabia ya Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-, akasema: Hivi si unasoma Qur'ani? Nikasema: Ndiyo! akasema: Basi tabia ya Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- ilikuwa ni Qur'ani.

[Sahihi] [Imepokelewa na Muslim katika ujumla wa hadithi iliyokuwa ndefu]

Aliulizwa mama wa waumini Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake- kuhusu tabia ya Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-, akajibu kwa neno lilokusanya, na akamuhamisha muulizaji upande wa Qura''ani tukufu iliyo kusanya sifa za ukamilifu, kama alivyosema -Rehema na amani ziwe juu yake- akasema alikuwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- akiiga tabia za Qur'ani, iliyoyaamrisha Qur'ani anayaamrisha, na yale inayoyakataza Qur'ani anayaepuka, basi ikawa tabia yake ni kuifanyia kazi Qur'ani, na kusimama katika mipaka yake na kua na adabu na adabu zake kuizingatia Qur'ani na matendo kwa ujumla na mfano wake.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/8265